

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MAGARI NA MALI CHAKAVU

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka "DART" unapenda kuutangazia Umma kwamba, utauza kwa njia ya mnada wa hadhara magari manne (4) aina ya "Ford" na vifaa chakavu vikiwemo samani za ofisi, vifaa vya TEHAMA na vifaa vingine.

Mnada utafanyika mnamo tarehe 7 Januari 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika ofisi za Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka zilizopo Ubungo Maji, Barabara ya Morogoro - Dar es Salaam. Mkabala na Ofisi za TANESCO Ubungo.

### MASHARTI YA MNADA

1. Mali zitauzwa kama zilivyo, mahali zilipo
2. Mnunuzi magari atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua **asilimia ishirini na tano (25%)** ya thamani ya mali husika na atatakiwa kukamilisha malipo yote katika muda wa **siku kumi na nne (14)** kuanzia tarehe ya mnada.
3. Mnunuzi atatakiwa kubadilisha umiliki wa gari husika ndani ya kipindi cha miezi **mitatu (3)**.

4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua si chini ya **siku saba (7)** kuanzia siku ya kukamilisha malipo. Hii ni kwa magari tu. Aidha, kwa vifaa vya ofisi na vifaa vinginevyo, mnunuzi atatakiwa kukamilisha malipo na kuondoa/kuchukua chombo hicho siku ya mnada.
5. Ruhusa ya kuangalia magari na vyombo husika itatolewa kwa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada yaani tarehe **5 Januari 2023** na **tarehe 6 Januari 2023** kuanzia saa 04:00 asubuhi hadi saa **09:30** alasiri.
6. Mnada utaanza saa 04:00 asubuhi siku ya Jumamosi mnamo tarehe **7 Januari 2023**.
7. Vigezo na masharti ya mnada kuzingatiwa.
8. Tangazo la mnada pia linapatikana katika tovuti ya Wakala pamoja na kurasa za mitandao ya jamii (**DARTMwendokasi**)

**MTENDAJI MKUU**  
**WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA**

**12 DISEMBA 2022**

